JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001 : 2015 Certified

# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA SEKTA NDOGO YA MAFUTA KATIKA MKONDO WA KATI NA CHINI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24



**MACHI 2025**

# YALIYOMO

UJUMBE WA MWENYEKITI ........................................................................... iv
DIBAJI............... ..................................................................................... vi
VIFUPISHO VYA MANENO.........................................................................viii

**1. UTANGULIZI.......................................................................................1**

**2. MIUNDOMBINU YA MAFUTA .................................................................2**

2.1 Miundombinu ya Kupokelea Mafuta ......................................................2
2.2 Maghala ya Kuhifadhi Mafuta ...............................................................2
2.3 Miundombinu ya TAZAMA ....................................................................3
2.4 Miundombinu ya Kusafirisha Mafuta......................................................3
2.5 Vituo vya Mafuta ...................................................................................4

**3. UAGIZAJI, USAMBAZAJI NA MATUMIZI YA MAFUTA ..............................5**

3.1 Mfumo wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja (BPS) ...............................5
3.2 Kiasi cha Mafuta Kilichoingizwa Nchini.................................................5
3.3 Matumizi ya Mafuta...............................................................................6
3.4 Upatikanaji wa Mafuta ..........................................................................7

**4. BEI ZA MAFUTA.......................................................................................8**

4.1 Bei za Mafuta Ghafi ...............................................................................8
4.2 Bei za Mafuta katika Soko la Dunia .......................................................8
4.3 Bei za Mafuta katika Soko la Ndani ........................................................8
4.4 Gharama za Ucheleweshaji wa Meli.......................................................9
4.5 Ushindani katika Soko Miongoni mwa Kampuni za Mafuta ...................9

**5. MIUNDOMBINU NA USAMBAZAJI WA LPG ...........................................11**

5.1 Miundombinu ya LPG .......................................................................... 11
5.2 Uagizaji wa LPG ................................................................................... 11
5.3 Mwenendo wa Bei za LPG katika Soko la Dunia..................................12
5.4 Nishati Safi ya Kupikia .........................................................................12
5.5 Ushindani wa Soko kwa Kampuni zinazofanya Biashara ya LPG .......14

**6. MIUNDOMBINU YA VILAINISHI NA USAMBAZAJI WAKE ........................15**

6.1 Shughuli za Vilainishi na Miundombinu ..........................................15
6.2 Usambazaji wa Vilainishi Tanzania Bara ..........................................16

**7. VIBALI VYA UJENZI NA LESENI.........................................................17**

7.1 Utoaji wa Vibali vya Ujenzi.................................................................17
7.2 Utoaji wa Leseni ..................................................................................18

**8. USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA............................................19**

8.1 Kufuatilia Uzingatiaji wa Viwango vya Miundombinu ya Mafuta ..........19
8.2 Kufuatilia Ubora wa Mafuta.................................................................19
8.3 Programu ya Vinasaba kwenye Mafuta ..............................................21
8.4 Uzingatiaji wa Kanuni za Kukokotoa Bei za Mafuta............................22

**9. UTEKELEZAJI WA MRADI WA EACOP.................................................23**

**10. TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA NA UKAGUZI WA MAZINGIRA ..25**

**11. UCHUNGUZI WA MATUKIO NA AJALI ..................................................26**

**12. MATOKEO YA UDHIBITI ........................................................................28**

**13. CHANGAMOTO KATIKA SEKTA NDOGO YA MAFUTA...........................29**

**14. MTAZAMO WA BAADAYE WA SEKTA NDOGO YA MAFUTA..................30**

**15. HITIMISHO..............................................................................................31**

# UJUMBE WA MWENYEKITI

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, nina furaha kuwasilisha Taarifa ya 10 ya Utendaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta katika Mkondo wa Kati na Chini kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Taarifa hii inatoa muhtasari wa utendaji wa sekta ndogo ya mafuta kwa upande wa Tanzania Bara na inajumuisha maelezo kuhusu vipengele mbalimbali vya sekta hii, kama vile mfumo wa kisheria unaosimamia sekta ndogo ya mafuta; miundombinu inayohusisha shughuli za mafuta; kampuni zinazoleta mafuta nchini kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja (BPS); kiasi cha mafuta kilichoagizwa kutoka nje; umiliki wa soko kwa kampuni zinazofanya biashara ya mafuta nchini; mwenendo wa bei za mafuta; uzingatiaji wa sheria, taratibu, kanuni na viwango vya kimataifa vinavyosimamia biashara ya mafuta nchini. Taarifa hii inalenga kuongeza uelewa wa hali ya sasa ya utendaji wa sekta ndogo ya mafuta.

EWURA imeendelea kutekeleza majukumu yake ya udhibiti wa kiufundi na kiuchumi katika sekta ndogo ya mafuta ikiwa ni pamoja na kuhakikisha usambazaji thabiti na uhakika wa upatikanaji wa mafuta kote nchini; kufuatilia uzingatiwaji wa sheria, taratibu na kanuni zinazosimamia biashara ya mafuta nchini; kuhakikisha kuwa kampuni zinazodhibitiwa zinafuata viwango vya juu vya udhibiti na uendeshaji; kuhamasisha ujenzi wa vituo vya mafuta kwa gharama nafuu katika maeneo ya vijijini na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia gesi ya kupikia (LPG). Juhudi hizi za kuongeza uwezo wa kuhifadhi gesi ya kupikia zinaendana na lengo la Serikali la kuhamia kwenye nishati safi ya kupikia. Kupitia mipango hii, EWURA iliendelea kuimarisha ufanisi na usalama wa sekta ndogo ya mafuta huku ikichangia katika malengo mapana ya uhifadhi wa mazingira na matumizi ya nishati safi.

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, hali ya upatikanaji wa mafuta nchini ilikuwa ya kuridhisha licha ya changamoto zilizojitokeza ikiwa ni pamoja na upungufu wa fedha za kigeni sokoni na uwezo mdogo wa miundombinu ya kupakua mafuta katika Bandari ya Da es Salaam ambayo ndiyo bandari kuu inayopokea mafuta nchini. Ubora wa vituo vya mafuta umeendelea kuimarishwa kwa kuzingatia taratibu madhubuti za utoaji leseni na ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha sheria, taratibu na kanuni zinafuatwa. Zaidi ya hayo, kumekuwa na ongezeko kubwa la uwekezaji wa vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini, jambo linaloakisi dhamira ya kusaidia ukuaji wa shughuli za uchumi na kijamii katika miji na vijiji.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Nishati kwa ushirikiano na mwongozo katika utekelezaji wa kazi ya udhibiti inayofanywa na EWURA katika sekta ndogo ya mafuta. Aidha, ninawapongeza wafanyabiashara wote katika sekta

hii kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha, kwani juhudi zao zimesaidia kudumisha na kuleta maendeleo katika ya sekta ndogo ya mafuta.

Mwisho, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Bodi ya EWURA, Menejimenti na Wafanyakazi wa EWURA kwa kujitoa kwao na michango yao ya busara katika maendeleo ya sekta ndogo ya mafuta. Juhudi na bidii zao zimekuwa mhimili wa kuendeleza malengo ya EWURA na kukuza sekta ndogo ya mafuta katika mkondo wa kati na wa chini Tanzania Bara.

--------------------------------------

Prof. Mark J. Mwandosya

**MWENYEKITI WA BODI**

# DIBAJI

Sheria ya Petroli, Sura ya 392, pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Sura ya 414, zinatoa msingi wa kisheria wa kudhibiti sekta ndogo ya mafuta katika mkondo wa kati na chini, Tanzania Bara. Sheria hizi, pamoja na kanuni na miongozo mbalimbali, zinatoa mwongozo wa usimamizi wa shughuli za mafuta katika mkondo wa kati na chini. Kwa mujibu wa Kifungu cha 30(1) cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392, EWURA ina jukumu la kufanya kazi za udhibiti wa kiufundi, kiuchumi na usalama katika uendeshaji wa biashara ya mafuta katika mkondo wa kati na chini. Aidha, Kifungu cha 31(2)(b) cha Sheria ya Petroli kinaiagiza EWURA kuandaa taarifa ya mwaka ya shughuli za mafuta. EWURA imeandaa taarifa hii ya mwaka inayoelezea utendaji wa sekta ndogo ya mafuta katika mkondo wa kati na chini kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 kuanzia Julai 2023 hadi Juni 2024. Muhtasari wa utendaji wa sekta hii kwa Mwaka wa Fedha uliomalizika tarehe 30 Juni 2024 ni kama ifuatavyo:

(a) Uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi uliongezeka kwa asilimia 12.1 kutoka lita bilioni 8.23 zilizoagizwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi lita bilioni 9.22 zilizoagizwa katika Mwaka wa Fedha 2023/24. Uagizaji wa bidhaa za mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani uliongezeka kwa asilimia 10.9, kiwango kinachoakisi ukuaji wa uchumi kutokana na ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia 5.1 mwaka 2023 na kutarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.7 mwaka 2024. Uagizaji wa mafuta yanayoenda nchi jirani kupitia Tanzania uliongezeka kwa asilimia 13.1 kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam na Tanga katika uingizaji wa mafuta kuelekea nchi jirani zisizo na bandari.

(b) Uagizaji wa gesi ya kupikia (LPG) uliongezeka kwa asilimia 16 kutoka tani 293,167 zilizoagizwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi tani za ujazo 403,638 zilizoagizwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Kuzinduliwa kwa Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia na Wizara ya Nishati mnamo mwezi Novemba 2022 na programu zinazoendelea za kuongeza wigo wa soko zinazofanywa na kampuni za LPG (LMCs) kulichangia kuongezeka kwa uagizaji wa LPG.

(c) Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, lita milioni 61.2 za vilainishi zilisambazwa sokoni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.2 kutoka lita milioni 59.3 zilizotolewa Mwaka wa Fedha 2022/23. Kati ya vilainishi vyote vilivyosambazwa, asilimia 83 vilizalishwa kwenye mitambo ya kuchakata vilainishi inayofanya kazi nchini, huku asilimia 19 iliyobaki ikiagizwa kutoka nje.

(d) Wastani wa bei ya mafuta ghafi kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23 ilikuwa Dola za Marekani 84 kwa pipa, ikionesha kupungua kwa asilimia mbili kutoka wastani ya Dola za Marekani 86 kwa pipa katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23. Kupungua huku kunahusishwa na sababu kadhaa, ikiwa ni pamoja na kudorora kwa uchumi wa dunia, kuongezeka kwa viwango vya uzalishaji na mivutano ya siasa za kidunia.

(e) Kwa wastani, bei za mafuta katika soko la dunia kwa petroli, dizeli na mafuta ya ndege/mafuta ya taa zilishuka kwa asilimia 0.5, 8 na 6 mtawalia mwaka 2023/24 ikilinganishwa na wastani wa bei katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23. Kushuka kwa bei hizi kunatokana na kushuka kwa bei ya mafuta ghafi.

EWURA iliendelea kusimamia sekta ndogo ya mafuta katika mkondo wa kati na chini, na kuhakikisha mfumo wa biashara hii unakuwa shwari na kuna uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta kwa mwaka mzima. Mamlaka ilifanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, kanuni na viwango vya ubora vilivyoainishwa katika biashara ya mafuta nchini.

Taarifa hii inalenga kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika sekta ndogo ya mafuta katika mkondo wa kati na ya chini, hasa kwa kuboresha na kujenga miundombinu mipya, ikiwa ni pamoja na miundombinu ya kupokea, kuhifadhi na vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini. Ni matumaini yangu kuwa wadau wetu wataitumia taarifa hii katika kufanya maamuzi yao katika uwekezaji na mipango mbalimbali ya siku zijazo.

---------------------------------------------

Dkt. James Andilile Mwainyekule

**MKURUGENZI MKUU**

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| ATGs | Mfumo wa kupima mafuta kwenye matanki |
| BPS | Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja |
| EA | Ukaguzi wa Mazingira |
| EACOP | Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki |
| EIA | Tathmini ya Athari kwa Mazingira |
| EWURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| GIS | Geographic Information System |
| GN | Tangazo la Serikali |
| HFO | Mafuta Mazito |
| HSE | Afya, Usalama na Mazingira |
| IDO | Dizeli ya Viwandani |
| KOJ1 | Kurasini Oil Jetty 1 |
| KOJ2 | Kurasini Oil Jetty 2 |
| LPG | Gesi ya kupikia |
| NEMC | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira |
| OMCs | Kampuni zinazoagiza na kuuza Mafuta kwa Jumla |
| LMCs | Kampuni zinazoagiza na kuuza LPG kwa Jumla |
| OPEC | Muungano wa Nchi Zinazozalisha Mafuta |
| PBPA | Wakala wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja |
| REA | Wakala wa Nishati Vijijini |
| SBM | Single Buoy Mooring |
| TAZAMA | Bomba la Mafuta la Tanzania na Zambia |
| TBS | Shirika la Viwango Tanzania |
| TIPER | Kampuni ya TIPER |
| TPA | Mamlaka ya Bandari Tanzania |
| TPDC | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |

# 1. UTANGULIZI

Kifungu cha 30(1) cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392, kimekasimu kwa EWURA wajibu wa kufanya kazi za udhibiti wa kiufundi, uchumi na usalama wa shughuli za mafuta kwenye mkondo wa kati na chini, Tanzania Bara. Mamlaka inahakikisha kuwa sekta ndogo ya mafuta inafanya kazi vizuri na kwa haki. Udhibiti madhubuti husaidia kudumisha viwango, kukuza na kuongeza uwazi, na kuhakikisha ufanisi, mambo muhimu kwa ukuaji na udhibiti wa sekta yoyote.

Taarifa hii ya Utendaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta katika Mkondo wa Kati na Chini kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 ni toleo la 10 la taarifa hizi ambazo huchapishwa na EWURA kila mwaka. Taarifa hii inatoa takwimu za kina na uchambuzi kuhusu sekta ndogo ya mafuta katika mkondo wa kati na wa chini Tanzania Bara kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Pia taarifa hii inatoa ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na miundombinu ya mafuta, taratibu za uagizaji wa mafuta, mwenendo wa matumizi ya mafuta, mwenendo wa bei katika soko la kimataifa na la ndani na shughuli za udhibiti na uzingatiaji wa matakwa ya leseni, viwango vya ubora kitaifa, mazingira na mahitaji ya usalama.

# 2. MIUNDOMBINU YA MAFUTA

Miundombinu mikuu iliyopo nchini kwa ajili ya shughuli za mafuta katika sekta ndogo ya mafuta katika mkondo wa kati na wa chini ni pamoja na miundombinu ya kupakua mafuta kutoka kwenye meli za mafuta, maghala ya kuhifadhia mafuta, vyombo vya usafirishaji (meli, magari, mabomba na mabehewa ya treni), vituo vya mafuta, na miundombinu ya kuwekea mafuta kwenye vyombo vya majini. Tanzania ina miundombinu ya mafuta katika mnyororo mzima wa usambazaji yenye uhakika ili kuhakikisha mafuta yanayopokelewa bandarini yanafikishwa kwa watumiaji wa mwisho nchini au kusafirisha kwenda nchi jirani kwa ufanisi.

## 2.1 Miundombinu ya Kupokelea Mafuta

Mafuta huingizwa nchini kwa kutumia meli za mafuta ambazo hupokelewa kupitia Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, kwa ajili ya matumizi ya hapa nchini na pia kusafirishwa kwenda nchi jirani zisizo na bandari ikiwemo Zambia, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Malawi, Rwanda na Burundi.

Mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani kupitia Bandari ya Mtwara ni kwa ajili ya mikoa ya Mtwara, Lindi, na Ruvuma, ambapo mafuta yanayoingizwa kupitia Bandari ya Tanga ni kwa ajili ya mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Manyara na Arusha. Bandari hizi mbili pia hupokea mafuta kwa ajili ya soko la nchi jirani, lakini Bandari ya Dar es Salaam ndiyo bandari kuu ya kupokea mafuta kwenda nchi jirani. Katika Bandari ya Dar es Salaam, Boya la SBM linaweza kumudu kupokea meli zenye uwezo wa tani 150,000 kwa dizeli, wakati KOJ1 inapokea meli zenye uwezo wa hadi tani 45,000 kwa petroli, mafuta mazito (HFO), mafuta ya taa, mafuta ya ndege na dizeli. Aidha, KOJ2 inaweza kupokea meli zenye uwezo wa tani 5,000 kwa LPG na inatumika kupakia petroli, dizeli, mafuta ya taa, na mafuta ya ndege kwa ajili ya Zanzibar. Bandari ya Tanga ina uwezo wa kupokea meli za uwezo wa tani 40,000, mahususi kwa dizeli, petroli na mafuta ya taa. Huko Mtwara, meli zenye uwezo wa tani 38,000 zinaweza kupokelewa, hasa kwa dizeli na petroli.

## 2.2 Maghala ya Kuhifadhi Mafuta

Sehemu hii inaangazia maghala ya kuhifadhi bidhaa za mafuta yaliyopo bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Kufikia tarehe 30 Juni 2024, kulikuwa na maghala 23 ya kupokea na kuhifadhi mafuta yenye uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 1,637,222 kwa wakati mmoja. Kwa sasa, kiwango cha matumizi ya mafuta nchini ni mita za ujazo 13,344.66 kwa siku. Kwa hivyo, maghala haya yanaweza kuhifadhi mafuta yanayokidhi mahitaji ya nchi kwa takriban siku 123. Hata hivyo,

iwapo mahitaji ya mafuta yanayopelekwa nchi jirani yatazingatiwa, kiwango cha matumizi kitakuwa mita za ujazo 26,797.43 kwa siku. Kwa hiyo, maghala yaliyopo yanaweza kuhifadhi mafuta ya kukidhi matumizi ya siku 61 kwa mafuta yote ya ndani na ya nje.

Vilevile, kuna maghala ya mafuta 28 katika maeneo mbalimbali nchini yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya mita za ujazo 70,937. Maghala haya yanaweza kupokea mafuta kutoka maghala yaliyopo Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kwa kutumia mabehewa ya treni na magari. Hata hivyo, kwa vile bidhaa nyingi za mafuta husafirishwa kwa barabara, matumizi ya maghala haya 28 yalionekana kuongeza gharama za uendeshaji. Kwa hiyo, maghala mengi kati ya haya hayafanyi kazi kwa sasa. Magari yanatumika kusafirisha bidhaa za mafuta moja kwa moja kutoka kwenye maghala yaliyoko Dar es Salaam, Tanga na Mtwara hadi kwenye vituo vya mafuta na miundombinu ya watumiaji binafsi.

## 2.3 Miundombinu ya TAZAMA

Miundombinu hii inajumuisha maghala ya kuhifadhia mafuta pamoja na bomba linalopokea na kusafirisha mafuta ya dizeli kutoka Kigamboni, Dar es Salaam hadi Ndola, Zambia. Miundombinu hii inaendeshwa na kampuni ya TAZAMA Pipelines Limited, ambayo inamilikiwa kwa pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (asilimia 33.3) na Serikali ya Jamhuri ya Zambia (asilimia 66.7). Bomba la TAZAMA ni miundombinu ya kimkakati kwa uchumi wa Zambia, na husafirisha takriban asilimia 70 ya mahitaji ya dizeli ya nchi hiyo. Bomba hilo lina urefu wa jumla ya kilomita 1,710. Aidha, maghala yake ya kuhifadhia mafuta yana uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 231,000.

TAZAMA Pipelines Limited inafanya upembuzi yakinifu ili kuongeza uwezo wake wa kuhifadhi mafuta kutoka mita za ujazo 231,000 hadi mita za ujazo 380,000 na kujenga bomba jipya litakaloweza kusafirisha mafuta zaidi kutoka Dar es Salaam hadi Ndola kupitia mkuza wa bomba lililopo. Bomba jipya litakuwa na matoleo katika miji ya Morogoro, Makambako, Mbeya na Songwe kwa ajili ya mafuta ya nchini Tanzania, pamoja na Mpika na Serenje nchini Zambia.

## 2.4 Miundombinu ya Kusafirisha Mafuta

Usafirishaji na usambazaji wa mafuta kutoka Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kwenda kwenye vituo vya mafuta nchini na nchi jirani hufanywa hasa kwa kutumia magari. Mabehewa ya treni pia hutumika kusafirisha bidhaa za mafuta. GBP Tanzania Limited husafirisha mafuta kutoka ghala lake la Tanga hadi maghala ya Kigoma na Mwanza kupitia njia ya reli ya kati inayopitia Tanga, Ruvu, Morogoro, Dodoma na Tabora.

## 2.5 Vituo vya Mafuta

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, kulikuwa na vituo vya mafuta 2,597 Tanzania Bara ikilinganishwa na 2,361 vilivyokuwepo tarehe 30 Juni 2023. Idadi hii ni sawa na ongezeko la asilimia 10. Kati ya vituo vyote hivyo, vituo 480 vinapatikana vijijini ambavyo vimeongezeka kwa asilimia 32.96 kutoka vituo 361 vilivyokuwepo hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023. Uwekezaji huu umechangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta nchini kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi zikiwemo kilimo, madini, ujenzi, shughuli za usafirishaji pamoja na uboreshaji mitandao ya barabara hasa maeneo ya vijijini. Serikali imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza uwekezaji wa vituo vyenye gharama nafuu katika maeneo ya vijijini.

# 3. UAGIZAJI, USAMBAZAJI NA MATUMIZI YA MAFUTA


## 3.1 Mfumo wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja (BPS)

Uagizaji wa bidhaa za mafuta kwa matumizi ya ndani unafanywa kupitia mfumo wa BPS unaoratibiwa na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA). Uagizaji wa bidhaa za mafuta kwa soko la nje unaweza kufanywa kupitia BPS au kwa mipango binafsi inayofanywa na mwagizaji. Bidhaa ambazo kwa sasa zinaagizwa kupitia BPS ni petroli, dizeli, mafuta ya taa na mafuta ya ndege. Bidhaa zingine za mafuta huagizwa kutoka nje kupitia mipango inayofanywa na waagizaji wenye leseni.

PBPA huratibu uagizaji wa mafuta kupitia zabuni za kitaifa na kimataifa zinazoshindanisha kampuni za kuleta mafuta zilizosajiliwa na PBPA. Ushindi kwa kila zabuni unategemea kampuni iliyowasilisha kiwango cha chini cha gharama za kuleta mafuta (*premiums*) kwa kila zabuni.

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, PBPA ilitangaza jumla ya zabuni 116 kwa waagizaji wa bidhaa za mafuta ambalo ni ongezeko la zabuni 9 kutoka zabuni 107 zilizotangazwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Ongezeko la idadi ya zabuni kunachangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta nchini na nchi jirani zinazotumia bandari za Tanzania. Kampuni zilizoshinda zabuni za kuleta mafuta ni Addax Energy (23), Sahara Energy (21), Augusta Energy (18), Coral Energy (18), Montfort Trading (14), E3 Energy (12), HAPCO (8), TPDC (1) na Vitol Bahrain (1).


Wastani wa *premiums* Mwaka wa Fedha 2023/24 ulipungua kwa asilimia 21.7 kwa dizeli, na kuongezeka kwa asilimia 0.6 na asilimia 4.5 kwa petroli na mafuta ya ndege/ mafuta ya taa mtawalia, ikilinganishwa na *premiums* za Mwaka wa Fedha 2022/23.




## 3.2 Kiasi cha Mafuta Kilichoingizwa Nchini

Mafuta yanayoagizwa kutoka nchi za nje ni petroli, dizeli, mafuta ya taa, mafuta ya ndege na mafuta mazito (HFO). Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, uagizaji wa mafuta uliongezeka kwa asilimia 12.1 kutoka lita bilioni 8.23 zilizoagizwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi lita bilioni 9.22 zilizoagizwa katika Mwaka wa Fedha 2023/24.

Ongezeko la mafuta yaliyoagizwa kutoka nje limechangiwa zaidi na ukuaji wa uchumi kutokana na ukuaji wa pato la taifa kwa asilimia 5.1 mwaka 2023 na unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.7 mwaka 2024. Uagizaji wa mafuta kwa ajili ya soko la ndani uliongezeka kwa asilimia 10.9 na uagizaji kwa ajili ya nchi jirani uliongezeka kwa asilimia 13.1. Kuongezeka mafuta kwenda nchi jirani kumechangiwa na kuongezeka kwa matumizi ya njia ya Tanzania kupitia Bandari za Dar es Salaam na Tanga. Uagizaji wa mafuta ya taa umeendelea kupungua huku vyanzo mbadala kama umeme, LPG na nishati ya jua vikichukua nafasi ya mafuta ya taa.




## 3.3 Matumizi ya Mafuta

Sehemu kuu za biashara zinazotumia bidhaa za mafuta ni usafirishaji, viwanda, ujenzi, uchimbaji wa madini, kilimo na anga. Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, jumla ya lita 4,633,211,564 za mafuta zilitumika ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 4.2 ikilinganishwa na lita 4,446,691,488 zilizotumika Mwaka wa Fedha 2022/23 kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali.**

**Jedwali: Matumizi ya Mafuta Mwaka wa Fedha 2023/24 (lita)**

| Mwaka | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Taa | HFO | Mafuta ya Ndege | IDO | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2023/24** | 2,580,133,240 | 1,753,290,950 | 9,161,600 | 27,496,150 | 263,109,624 | 20,000 | **4,633,211,564** |
| **2022/23** | 2,520,847,056 | 1,639,465,033 | 9,671,800 | 33,283,991 | 243,383,608 | 40,000 | **4,446,691,488** |
| **Mabadiliko** | **2.4%** | **6.9%** | **-5.3%** | **-17.4%** | **8.1%** | **-50.0%** | **4.2%** |

### 3.3.1 Matumizi ya Mafuta kwa kila Mkoa

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, matumizi ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kupitia vituo vya mafuta na miundombinu binafsi kwa ujumla yalifikia lita 4,342,585,790. Matumizi ya juu zaidi yalikuwa mkoa wa Dar es Salaam ukifuatiwa na Mwanza, Pwani, Arusha na Dodoma.

### 3.3.2 Matumizi ya Mafuta kwenye Shughuli za Anga


Huduma za mafuta kwenye shughuli za anga katika viwanja mbalimbali vya ndege nchini zilitolewa na kampuni nne zinazouza mafuta ya ndege ambazo ni

Puma Energy, TotalEnergies, Oilcom, na Lake Oil. Katika kipindi hiki, jumla ya lita 263,109,624 za mafuta ya ndege na lita 390,015 za *Aviation Gasoline (AvGas)* zilisambazwa. Puma Energy ilikuwa msambazaji pekee wa *AvGas*. Sehemu kubwa ya mafuta ya ndege ilitumika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), ikiwa ni asilimia 81.2 ya matumizi yote kutokana na shughuli nyingi za usafiri wa anga ikilinganishwa na viwanja vingine vya ndege, ukifuatiwa na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) wenye asilimia 13.0.

## 3.4 Upatikanaji wa Mafuta

Mamlaka iliendelea kusimamia hali ya upatikanaji wa mafuta kwa kuzingatia kanuni na. 6 ya *the Petroleum (General) Regulations of 2011* inayowataka wauzaji wa jumla wa mafuta kuwa na mafuta yanayotosheleza angalau siku 15. Aidha, kanuni na. 25(1)(I) ya *Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation) Rules 2022, GN 150* inawataka wauzaji wa jumla kuandaa na kuwasilisha bakaa ya mafuta ya kila wiki kwa EWURA. Zaidi ya hayo, Mamlaka inafanya kazi pamoja na PBPA ili kuhakikisha mafuta ya kutosha yananunuliwa kupitia BPS kila mwezi. Lengo kuu ni kuhakikisha upatikanaji wa mafuta yanayokidhi viwango vya ubora nchini wakati wote.

Katika kipindi husika, hapakuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa mafuta nchini. Hata hivyo, petroli, dizeli na LPG hazikukidhi takwa la kisheria la kuwa angalau na utoshelevu wa siku 15 kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 1.**





**Kielelezo Na. 1: Wastani wa akiba ya mafuta kwa Mwaka wa Fedha 2023/24**

Sababu kuu ya akiba ndogo ya petroli na dizeli ilikuwa uhaba wa Dola za Marekani kwa ajili ya malipo ya uagizaji wa mafuta ambayo pia ilisababisha kupokea kiasi kikubwa cha mafuta ambayo hayakuwa yamelipiwa baada ya kuwasili nchini. Serikali ilichukua hatua mbalimbali ikiwemo kuruhusu sarafu nyingine za kimataifa zikubalike kwenye malipo ya mafuta yaliyoagizwa kutoka nje, kuruhusu matumizi ya hedge instruments kama vile forwards contracts na swaps; na kuongeza financing cost kutoka asilimia 1 hadi asilimia 1.5 ya CIF. Kufikia mwisho wa robo ya nne ya Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, kiwango cha mafuta yaliyopokelewa bila kulipiwa kilipungua.

# 4. BEI ZA MAFUTA


## 4.1 Bei za Mafuta Ghafi

Wastani wa bei ya mafuta ghafi katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 ilikuwa Dola za Marekani 84.19 kwa pipa, ambayo ni pungufu ya asilimia 2 ikilinganishwa na wastani wa bei ya mafuta ghafi ya Dola za Marekani 86 kwa pipa katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23. Sababu kuu ya kupungua kwa bei ni uzalishaji wa ziada kuliko mahitaji.




## 4.2 Bei za Mafuta katika Soko la Dunia


Kwa wastani, bei za petroli, dizeli na mafuta ya ndege/mafuta ya taa katika soko la dunia zilishuka kwa asilimia 0.5, 8 na 6 mtawalia katika Mwaka wa Fedha 2023/24 ikilinganishwa na wastani wa bei katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23.




## 4.3 Bei za Mafuta katika Soko la Ndani


Bei za mafuta zinakokotolewa na kuchapishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 166 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392. Bei kikomo za jumla na rejareja za dizeli, petroli na mafuta ya taa zinakokotolewa kila mwezi kwa mujibu wa kanuni zinazoitwa *the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Products Price Setting) Rules, 2022*.

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, wastani wa bei za rejareja za mafuta jijini Dar es Salaam ulikuwa Shilingi 3,166 kwa lita ya petroli, Shilingi 3,128 kwa lita ya dizeli na Shilingi 3,030 kwa lita ya mafuta ya taa, ikiwa ni ongezeko la asilimia 5 kwa petroli, upungufu wa asilimia 2 na 5 kwa dizeli na mafuta ya taa, mtawalia ikilinganishwa na wastani wa bei ya mafuta katika Mwaka wa Fedha 2022/23.




## 4.4 Gharama za Ucheleweshaji wa Meli

Gharama za ucheleweshaji wa meli bandarini ni gharama zinazolipwa na waagizaji wa mafuta kutokana na ucheleweshaji wa kushusha mafuta yaliyoletwa kulingana na muda uliokubaliwa kwenye mkataba wa kuleta mafuta.




## 4.5 Ushindani katika Soko Miongoni mwa Kampuni za Mafuta

Mamlaka hufuatilia utendaji wa kampuni za uuzaji wa mafuta kwa jumla (OMCs) ili kufahamu hali ya ushindani katika soko. Katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, biashara ya mafuta nchini iliendelea kuwa ya ushindani. Puma Energy (asilimia 16.7), MOIL (asilimia 10.9), Oilcom (asilimia 6.7), TotalEnergies (asilimia 5.9), Mount Meru Petroleum (asilimia 5.8) na Lake Oil (asilimia 5.2) kwa pamoja walichangia asilimia 51.2 ya umiliki wa soko huku kampuni zaidi ya 35 zikigawana sehemu iliyobaki ya soko.


Puma Energy imeendelea kushika nafasi ya kwanza kwa mwaka wa tatu mfululizo huku MOIL ikitoka nafasi ya nne ikiwa na umiliki wa soko kwa asilimia 8.5 mwaka 2021 hadi kuwa ya pili kwenye soko kwa asilimia 11.12. Kampuni nyingine ambazo zimeongeza soko ni pamoja na Oilcom, Mount Meru Petroleum, na Lake Oil.

Umiliki wa soko wa TotalEnergies umeshuka kutoka asilimia 13 mwaka 2021 hadi 5.9 katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, hivyo kutoka nafasi ya pili hadi ya nne. Kadhalika, Oryx Energies imeshuka kutoka asilimia 7.5 mwaka 2021 hadi asilimia 5.1 Mwaka wa Fedha 2023/24, ikishuka kutoka nafasi ya tano hadi ya saba. GBP imepoteza sehemu kubwa ya soko, ikishuka kutoka asilimia 8.5 mwaka 2021 hadi 3.5 katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, ikishuka kutoka nafasi ya tatu hadi ya 11.

# 5. MIUNDOMBINU NA USAMBAZAJI WA LPG

## 5.1 Miundombinu ya LPG

Miundombinu ya LPG Tanzania Bara ni pamoja na miundombinu ya kupokea, kuhifadhi, na kujaza LPG kwenye mitungi na maghala ya kuhifadhia mitungi ya LPG kwa ajili ya usambazaji. LPG inaingizwa Tanzania kupitia Bandari za Dar es Salaam na Tanga ambapo uwezo wa kuhifadhi LPG jijini Dar es Salaam na Tanga uliongezeka kutoka tani za ujazo 15,750 Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi tani za ujazo 17,700 (2023/24), ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.38 kama inavyoonyeshwa kwenye **Kielelezo Na. 2**.





**Kielelezo Na. 2:** Ukuaji wa uwezo wa kuhifadhi LPG (katika tani) Tanzania Bara

Ukuaji huu wa uagizaji na matumizi ya LPG, hasa kwa kupikia, unachangiwa kwa kiasi kikubwa na Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 5.2 Uagizaji wa LPG

Biashara ya LPG iliendelea kukua ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, uagizaji wa LPG uliongezeka kwa asilimia 38 na kufikia tani za ujazo 403,638 ikilinganishwa na tani za ujazo 293,167 zilizoagizwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

Wadau wakuu ambao ni Serikali na kampuni za LPG waliendelea kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu na urahisi wa kutumia vyanzo safi vya nishati. **Kielelezo Na. 3** kinaonyesha mwenendo wa ukuaji wa uagizaji wa LPG (tani) kutoka mwaka 2015/16 hadi 2023/24.




**Kielelezo Na. 3:** Mwenendo wa uagizaji wa LPG (katika tani) kuanzia Mwaka wa Fedha 2015/16 hadi 2023/24

## 5.3 Mwenendo wa Bei za LPG katika Soko la Dunia

Bei za LPG katika la soko la dunia zilipanda na kushuka ambapo bei za *Butane* zilifikia bei ya juu ya Dola za Marekani 640 kwa tani moja mwezi Februari na Machi 2024, wakati *propane* ilifikia kiwango cha juu cha Dola za Marekani 630 kwa tani moja katika kipindi hicho. Bei za chini kabisa zilikuwa mwezi Julai 2023 kwa bidhaa zote mbili ambapo *propane* ilikuwa Dola za Marekani 457 kwa tani moja na *butane* kwa Dola za Marekani 447 kwa uzito huo huo.

## 5.4 Nishati Safi ya Kupikia

Tarehe 1 na 2 Novemba 2022, Wizara ya Nishati ilifanya Kongamano la Nishati Safi ya Kupikia ambalo liliwashirikisha wadau kujadili masuala yanayohusu nishati safi ya kupikia na kukusanya maoni na mapendekezo kuhusu suala hilo. Madhumuni ya kongamano hilo yalikuwa ni:

i. Kupata uelewa wa kuhusu nishati inayotumika zaidi kupikia na athari zake kwa afya, mwingiliano wa kijamii na mazingira;

ii. Kupata uzoefu kutoka nchi ambazo zinatumia nishati safi ya kupikia kwa kiwango kikubwa;

iii. Kujadili na kutathmini sera, teknolojia, rasilimali fedha na kanuni zinazohitajika ili Tanzania ifanikiwe katika lengo la kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia;

iv. Kubainisha jukumu la kila mdau katika kutekeleza lengo la matumzi ya nishati safi ya kupikia; na

v. Kuimarisha ushirikiano baina ya wadau wa nishati safi ya kupikia.

Katika Kongamano hilo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza yafuatayo:

i. Kuandaliwa kwa Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia;

ii. Kupitiwa kwa sera, mipango na mikakati iliyopo na kupendekeza mabadiliko yanayopaswa kufanywa ili kufanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia na kisha kuratibu utekelezaji wake; na

iii. Kuanzishwa Mfuko wa Nishati safi ya Kupikia ambao utatumika katika kujenga uelewa, kutoa ruzuku na fedha kwa ajili ya uwekezaji katika teknolojia, uvumbuzi, ubunifu, maendeleo na kukuza nishati safi ya kupikia.

Rais pia aliagiza taasisi zote za umma na binafsi zinazohudumia chakula kwa zaidi ya watu 300 kwa siku kuacha matumizi ya kuni na mkaa na kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo Januari 2024. Taasisi hizo ni pamoja na shule, vyuo mbalimbali na kambi za vyombo vya ulinzi na usalama.

Kwa kuzingatia upatikanaji wake, LPG ni mojawapo ya chanzo cha nishati ya kuleta mapinduzi ya nishati safi ya kupikia. Kutokana na hali hiyo, katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais, taasisi mbalimbali zimefunga miundombinu ya kupikia inayotumia LPG jambo ambalo limechangia ongezeko la asilimia 38 la uagizaji wa LPG. Serikali kupitia REA inatekeleza programu mbalimbali za kuwezesha taasisi na watu binafsi kutumia nishati safi ya kupikia. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara ya Nishati na EWURA nazo zilitekeleza programu mbalimbali za uelimishaji wananchi juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia. Hayo yalifanyika

kwenye maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Maonesho ya Nane Nane pamoja na kupitia vipindi vya redio na televisheni. Kwa lengo la kitaifa la asilimia 80 ya watu kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034, uagizaji wa LPG unatarajiwa kuendelea kuongezeka.

## 5.5 Ushindani wa Soko kwa Kampuni zinazofanya Biashara ya LPG

Mamlaka iliendelea kufuatilia utendaji wa Kampuni za LPG kulingana na viwango vya mauzo katika soko. Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Oryx Gas Tanzania Limited iliongoza katika soko kwa kuhudumia asilimia 35.2 ya soko ikifuatiwa na Taifa Gas Tanzania Limited na Manjis Gas Supply Company Limited zenye asilimia 32.1 na asilimia 15.8 ya soko, mtawalia.

Ushindani katika soko umeendelea kuongezeka na kupelekea soko la Oryx Gas Tanzania Limited kushuka kutoka asilimia 45.6 mwaka 2021 hadi asilimia 35.2 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 wakati soko la Taifa Gas Tanzania Limited liliongezeka kutoka asilimia 22.7 hadi asilimia 32.1 na Manjis Gas Supply Company Limited kuongezeka kutoka asilimia 11.1 hadi asilimia 15.8. Mchango wa kampuni nyingine katika soko ni kama ifuatavyo: O-Gas asilimia 7.9, Lake Gas Limited asilimia 5.7, Orange Gas Tanzania Limited asilimia 1.9, Cam Gas asilimia 0.7, Puma Gas asilimia 0.4 na Mount Meru Gas asilimia 0.3.

# 6. MIUNDOMBINU YA VILAINISHI NA USAMBAZAJI WAKE

## 6.1 Shughuli za Vilainishi na Miundombinu

EWURA inasimamia usambazaji wa vilainishi Tanzania Bara ili kuhakikisha usalama, ubora na upatikanaji wake kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia usambazaji wa bidhaa hiyo. Vilainishi vinapatikana kwa njia mbili ambazo ni kuagiza nje vilainishi vilivyokamilika kwa matumizi sokoni na kuagiza malighafi hasa *base oil* kwa ajili ya kuchakata hapa nchini ili kupata vilainishi sahihi.

### 6.1.1 Miundombinu ya Kuchakata Vilainishi

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, kulikuwa na mitambo saba ya kuchakata vilainishi Tanzania Bara. EWURA inakagua miundombinu hii ili kuhakikisha kuwa inazingatia sheria, viwango, mahitaji ya afya usalama na mazingira (HSE) na taratibu nyingine bora za sekta ya mafuta kabla ya kuruhusiwa kufanya shughuli za biashara ya vilainishi.

### 6.1.2 Usajili wa Vilanishi

EWURA inasimamia shughuli za biashara ya vilainishi kupitia Kanuni za *Petroleum (Lubricants Operations) Rules 2022, GN 115*. Kanuni hizi zimekuwepo tangu 2014 na zimekuwa zikifanyiwa marekebisho mara kwa mara ili kuzingatia mahitaji ya wateja, kuimarisha utekelezaji na kuendana na mabadiliko ya teknolojia. Kanuni hizi zinamtaka mtu yeyote anayefanya biashara ya vilainishi Tanzania Bara kuwa na leseni ya EWURA.


EWURA inasajili vilainishi vilivyochakatwa nchini na vile vilivyoagizwa kutoka nje ya nchi ili kuzuia upatikanaji wa bidhaa duni zisizokuwa na ubora sokoni. Utaratibu huu husaidia katika kutambua na kufuatilia vilainishi kwenye soko, kuhakikisha ubora wa bidhaa, na kufuatilia bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora. Usajili unafanywa kwa kujaza fomu ya maombi ya usajili wa vilainishi na kuwasilisha uthibitisho kama ilivyoainishwa kwenye **Kielelezo Na. 4.**




**Kielelezo Na. 4:** Mahitaji kwa ajili ya usajili wa vilainishi

## 6.2 Usambazaji wa Vilainishi Tanzania Bara

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, jumla ya lita 61,133,024.55 za vilainishi zilisambazwa sokoni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 3 kutoka lita 59,306,966 zilizosambazwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Vilainishi vilivyochakatwa nchini vilikuwa lita 51,085,925.09 ikiwa ni asilimia 84 ya vilainishi vilivyosambazwa. **Kielelezo Na. 5** kinaonesha mchango wa kila mwezi wa vilainishi vilivyoagizwa kutoka nje na vilivyochakatwa nchini katika Mwaka wa Fedha 2023/24.




**Kielelezo Na. 5:** Uwiano wa Vilainishi Vilivyochakatwa Ndani na Vilivyoagizwa kutoka nje Kila Mwezi Mwaka 2023/24


# 7. VIBALI VYA UJENZI NA LESENI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 131(1) cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392, mtu yeyote anayetaka kufanya shughuli inayodhibitiwa lazima aombe leseni kutoka EWURA. Aidha, kifungu cha 126(1) cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392, kinamtaka mtu yeyote anayekusudia kujenga miundombinu ya bidhaa za mafuta ya petroli kuomba na kupata kibali cha ujenzi kutoka EWURA. Kifungu cha 127(1) cha Sheria ya Petroli Sura ya 392 kinakataza ujenzi wa mitambo ya petroli bila kibali kutoka EWURA. Kujenga miundombinu ya mafuta bila kibali ni kosa linaloadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

Maombi ya leseni na vibali vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta hufanywa kupitia mfumo wa License and Order Information System (LOIS) wa EWURA unaopatikana kupitia tovuti ya EWURA, yaani, www.ewura.go.tz.

## 7.1 Utoaji wa Vibali vya Ujenzi

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Mamlaka iliendelea kutoa vibali vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta ya petroli. Mamlaka ilitoa jumla ya vibali vya ujezi 300. Kati ya vibali vilivyotolewa, viwili vilikuwa kwa ajili ya vituo vya mafuta kwa matumizi binafsi, kimoja kwa ajili ya mitambo ya kuhifadhi na kujaza gesi ya kupikia, viwili kwa ajili ya miundombinu ya kupakia na kupokea mafuta baharini, 294 kwa ajili ya vituo vya mafuta na kibali kimoja kwa ajili ya miundombinu ya kuhifadhia mafuta ya petroli. Kati ya vibali vya ujenzi 294 vya vituo vya mafuta, vibali 175 vilikuwa kwa ajili ya vituo vya mafuta vya mijini na vibali 119 ni kwa ajili ya vituo vya mafuta vya vijijini. **Kielelezo Na. 6** kinaonyesha mwenendo wa idadi ya vibali vya ujenzi vilivyotolewa tangu 2017/18.




**Kielelezo Na. 6**: Idadi ya vibali vya ujenzi vilivyotolewa tangu Mwaka wa Fedha 2017/18 mpaka 2023/24

## 7.2 Utoaji wa Leseni

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Mamlaka ilitathmini na kutoa leseni 846 za biashara ya mafuta, zikiongezeka kutoka leseni 520 zilizotolewa Mwaka wa Fedha 2022/23. Kati ya leseni 846, leseni 319 zilitolewa kwa waombaji wapya, na 527 zilihuishwa. Pia, katika kipindi husika, Mamlaka ilisajili kampuni tatu (3) kama wakaguzi wa kujitegemea wa mafuta baharini.


# 8. USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, EWURA ilifuatilia utekelezaji wa sheria ili kuhakikisha kuwa wafanyabiashara katika sekta hii ndogo ya mafuta wanafuata sheria, kanuni, viwango na utendaji bora wa sekta. Juhudi hizi za ufuatiliaji zilijumuisha uchukuaji wa sampuli za mafuta ili kuthibitisha ubora, kusimamia mradi wa kuweka na kutambua vinasaba kwenye mafuta, kukagua miundombinu ya mafuta ili kuona iwapo inakidhi viwango vya miundombinu na mahitaji ya afya, usalama na mazingira (HSE), na kufuatilia uzingatiaji wa bei kikomo za mafuta. Wafanyabiashara waliobainika kukiuka sheria na viwango vinavyotumika walikabiliwa na hatua za kisheria

## 8.1 Kufuatilia Uzingatiaji wa Viwango vya Miundombinu ya Mafuta


Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Mamlaka ilikagua utekelezaji wa sheria, kanuni, viwango, masharti ya leseni na utendaji bora wa sekta husika katika miundombinu 840 ya mafuta. Kati ya miundombinu hiyo, miundombinu 666, sawa na asilimia 79.29 ilikidhi sheria, kanuni, viwango, masharti ya leseni na utendaji bora. Kiwango cha uzingatiaji kilipungua kwa asilimia 3.43, ikilinganishwa na kiwango cha uzingatiaji cha asilimia 82.72 kilichopatikana katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Waendeshaji wa miundombinu ambayo haikukidhi matakwa ya sheria, kanuni, viwango, masharti ya leseni na utendaji bora walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

## 8.2 Kufuatilia Ubora wa Mafuta



Kwa mujibu wa kifungu cha 30(2)(b) cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392, Mamlaka ina jukumu la kusimamia viwango vya ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli. Zaidi ya hayo, kifungu cha 179(1) cha Sheria hiyo hiyo kinataka bidhaa za mafuta ya petroli kukidhi ubora, usalama na viwango vya kimazingira vilivyowekwa na kanuni zilizowekwa na Waziri mwenye dhamana.

Mamlaka inafanya kaguzi za ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli kwa mujibu wa Kanuni za Mafuta (Uchukuaji wa Sampuli na Upimaji) za mwaka 2010, Gazeti la Serikali Na. 211. Katika kipindi cha mapitio, Mamlaka ilikusanya sampuli 763 za mafuta ya petroli kutoka kwenye vituo vya mafuta na ghala za kuhifadhi mafuta. Kati ya sampuli 763 zilizokusanywa, sampuli 729 sawa na asilimia 95.54 zilikidhi viwango vya ubora. Hatua za kisheria zilichukuliwa dhidi ya waendeshaji wa miundombinu ambao mafuta yao hayakukidhi viwango vinavyotakiwa, kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 179(2)(a) na (c) cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392. Hatua hizi ni pamoja na kufungwa kwa miundombinu husika na kutozwa faini.





**Kielelezo Na. 7:** Asilimia ya sampuli za mafuta ambazo hazikukidhi viwango vya ubora kutoka Mwaka wa Fedha 2010/11 hadi 2023/24

## 8.3 Programu ya Vinasaba kwenye Mafuta



Mamlaka iliendelea kutekeleza programu ya uwekaji vinasaba katika mafuta yanayotumika Tanzania Bara. Pamoja na mambo mengine, programu hii husaidia kubaini vituo vya mafuta vinavyouza mafuta yasiyolipiwa kodi na tozo stahiki za Serikali na hivyo kuathiri ushindani wa waki katika biashara ya mafuta. Hii hutokea pale ambapo mafuta yaliyotakiwa kwenda nchi jirani yakauzwa nchini, kwani mafuta hayo hayalipiwi kodi. Programu hii inasaidia Serikali kukusanya mapato stahiki na kushamirisha ushindani wa haki katika biashara ya mafuta.

Mamlaka ilifanya ukaguzi wa mara kwa mara na wa dharura, ikiwa ni pamoja na kuchukua sampuli za mafuta kutoka kwa waendeshaji mbalimbali wa vituo vya mafuta Tanzania Bara, ili kufanya vipimo vya kutambua viwango vya vinasaba katika mafuta. Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, vinasaba vilipimwa katika vituo 764 na vituo 738 ambavyo ni asilimia 96.59 vilikutwa na mafuta yenye viwango stahiki vya vinasaba. Vituo vilivyokutwa na mafuta yasiyo na viwango stahiki vya vinasaba vilichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. **Kielelezo Na. 8** kinaonyesha mwenendo wa asilimia ya vituo vilivyofeli kuwa na viwango stahiki vya vinasaba kutoka Mwaka wa Fedha 2010/11 hadi 2023/24.





**Kielelezo Na. 8:** Asilimia ya vituo vilivyofeli kuwa na viwango stahiki vya vinasaba kutoka Mwaka wa Fedha 2010/11 hadi 2023/24

## 8.4 Uzingatiaji wa Kanuni za Kukokotoa Bei za Mafuta

Kwa mujibu wa Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji za Ukokotoaji wa Bei za Mafuta, Mamlaka iliendelea kusimamia bei kikomo za petroli, dizeli na mafuta ya taa. Bei hizi zinakokotolewa na kuchapishwa Jumatano ya kwanza ya kila mwezi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, jumla ya vituo vya mafuta 846 vilikaguliwa kuthibitisha uzingatiaji wa bei kikomo zinazochapishwa kila mwezi. Wakati wa ukaguzi, vituo sita (6), sawa na asilimia 0.71 ya vituo viliyokaguliwa, vilipatikana vikiuza mafuta juu ya bei kikomo zilizochapishwa. Hatua za kisheria zilichukuliwa dhidi ya vituo hivyo.

# 9. UTEKELEZAJI WA MRADI WA EACOP

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) ulianzishwa kufuatia ugunduzi wa mafuta ghafi nchini Uganda mwaka 2006 unaokadiriwa kuwa mapipa bilioni 9. Hata hivyo, mafuta yanayoweza kuzalishwa kwa teknolojia iliyopo yanakadiriwa kuwa mapipa bilioni 6. Bomba hili la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga nchini Tanzania lina urefu wa kilomita 1,443. Kilomita 1,147 ziko Tanzania na kilomita 296 ziko Uganda. Ujenzi wa bomba hilo unatarajiwa kuanza Agosti 2024 na kukamilika ndani ya miezi 36. **Kielelezo Na. 9** kinaonesha mkuza wa EACOP nchini Uganda na Tanzania.




**Kelelezo Na. 9:** Mkuza wa EACOP kuanzia nchini Uganda hadi Tanzania

Mradi wa EACOP unaendelea na uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kufikia tarehe 30 Juni 2024, maendeleo ya jumla ya Mradi huu yalifikia asilimia 39.2, na jumla ya wananchi 9,827 walioathiriwa na Mradi, sawa na asilimia 99 walikuwa wamelipwa fidia. Fidia imefanyika kwa malipo ya fedha taslimu na utoaji wa nyumba mbadala. Nyumba zote mbadala 340 zimekamilika na kukabidhiwa kwa wahusika.

Katika kipindi husika, Mradi wa EACOP ulikuwa umetoa jumla ya fursa za ajira 4,865 kwa raia wa Tanzania chini ya mikataba ya muda mfupi na mrefu. Watanzania walioajiriwa moja kwa moja chini ya EACOP Limited walikuwa 184, wakati walioajiriwa na Wakandarasi daraja la kwanza wa EACOP Limited walikuwa 3,859 na walioajiriwa na EACOP *Corporate Contractors* walikuwa 822. **Kielelezo Na. 10** kinaonyesha maendeleo ya ujenzi wa EACOP, Handeni, Tanzania.



**Kielelezo Na. 10** Maendeleo ya ujenzi wa EACOP, Handeni, Tanzania

# 10. TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA NA UKAGUZI WA MAZINGIRA

Wawekezaji kwenye miradi wanatakiwa kufanya Tathmini ya Athari ya Mazingira (EIAs) na ukaguzi wa mazingira (EAs) ili kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Kanuni zake. EIAs lazima zifanyike kabla ya utekelezaji wa mradi wakati EAs zinafanywa baada ya kuanza kwa mradi na kutathmini mapendekezo ya utekelezaji wa mradi na matokeo ya mradi kwa mazingira.

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Mamlaka ilipokea na kupitia taarifa 163 za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) na taarifa 16 za Ukaguzi wa Mazingira (EA) zinazohusiana na miundombinu ya mafuta. EWURA itaendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kufanya EIA ili kulinda mazingira na kukidhi mahitaji ya kupata kibali cha ujenzi kutoka kwa Mamlaka.

# 11. UCHUNGUZI WA MATUKIO NA AJALI

Katika kipindi cha mapitio, Mamlaka ilichunguza matukio hatarishi ili kubaini chanzo na sababu zake na kupendekeza hatua za kurekebisha, kwa lengo la kuzuia matukio kama hayo siku za usoni. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 30(2)(o) cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392, kinachoitaka Mamlaka kufanya uchunguzi wa matukio yanayosababisha uharibifu wa miundombinu, majeruhi, kupoteza maisha au mali.

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, matukio nane yaliripotiwa yakihusisha hujuma za miundombinu ya bomba za mafuta kwa lengo la kuiba, uvujaji wa bomba la mafuta la TAZAMA, ajali za barabarani zilizohusisha lori zilizobeba mafuta na biashara kufanywa kinyume cha sheria. Taarifa zaidi za matukio hayo ni kama ifuatavyo:

i. Kuvuja kwa bomba la mafuta la kuelekea World Oil Terminal II Kigamboni, Dar es Salaam baada ya kutobolewa ili kuiba mafuta ya dizeli. Hii ilisababisha uchafuzi mkubwa wa mazingira kutokana na kumwagika kwa mafuta.

ii. Kutobolewa kwa bomba la TAZAMA maeneo ya Mbuyuni, wilaya ya Kilolo mkoani Iringa na kuibiwa kwa mafuta ya dizeli. Uhujumu huu wa bomba ulisababisha hasara ya upotevu wa mafuta kwa TAZAMA.

iii. Kupasuka kwa bomba la TAZAMA eneo la Mbagala - Kingugi, Temeke, Dar es Salaam na kusababisha uvujaji wa dizeli katika eneo hilo. TAZAMA ilidhibiti uvujaji wa mafuta, ilikarabati eneo la bomba lililopasuka na kusafisha mazingira yaliyoathirika na kuvuja kwa mafuta.

iv. Ajali iliyotokea katika eneo la Undomo, Kata ya Uchama, Nzega, Tabora iliyohusisha basi la Kampuni ya Alfa lenye namba za Usajili T612 CQD na lori la mafuta lenye namba za Usajili T481 AEB/T526 AEB, Ajali hii ilisababisha vifo vya watu nane, majeruhi 60 na uharibifu wa mazingira.

v. Ajali ya kupinduka kwa lori la mafuta eneo la Misugusugu, wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani kutokana na utelezi wa barabara uliosababishwa na mvua kubwa. Ingawa mifuniko ya tanki la lori ilibakia imara bila kuvuja kwa mafuta, wakazi wa eneo hilo walifungua vifuniko vya juu vya tanki, na kusababisha kumwagika kwa lita 18,000 za petroli, uharibifu wa barabara, na uchafuzi wa mazingira.

vi. Ajali ya kupinduka kwa lori la mafuta lenye namba za usajili T697DNE/ T981 DEL eneo la Kitembo, wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani. Ajali hiyo ilisababisha hasara ya kumwagika kwa lita 3,130 za mafuta na uharibifu wa barabara na lori.

vii. Lori lenye namba za Usajili T308 BBS liliwekwa kizuizini katika Kituo cha Polisi cha Barabara ya Kilwa, wilaya ya Temeke, mkoani Dar es Salaam, kwa tuhuma za kubeba mafuta ya wizi. Vipimo vya kugundua vinasaba kwenye mafuta vilionesha kuwa lori hilo lilikuwa limebeba mafuta yasiyo na vinasaba ikiashiria mafuta hayo hayakulipiwa kodi. Taarifa iliwasilishwa TRA kwa ajili ya hatua zaidi kwa mujibu wa Sheria za Kodi.

viii. Mfanyabiashara alikutwa eneo la Kurasini, Temeke akinunua mafuta kutoka kwenye lori za mafuta na kuuza kwenye lori ndogo zinazosambaza mafuta kinyume cha sheria.

# 12. MATOKEO YA UDHIBITI

Kupitia hatua mbalimbali za udhibiti zilizochukuliwa, EWURA imeleta matokeo makubwa katika sekta ndogo ya mafuta katika mkondo wa kati na chini katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Matokeo hayo ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa uzingatiaji wa sheria, kanuni na viwango vya ubora wa miundombinu na bidhaa za mafuta.

ii. Ongezeko la kiasi cha vilainishi vilivyosambazwa huku asilimia 84.3 ya vilainishi hivyo ikiwa imezalishwa katika viwanda vya kuchanganya vilainishi vilivyopo hapa nchini. Hii inaakisi ukuaji wa sekta ya uzalishaji wa ndani.

iii. Kulinda watumiaji wa mafuta kwa kutangaza bei kikomo za mafuta zinazoakisi gharama halisi. EWURA ilisimamia utekelezaji wa bei kikomo za mafuta na kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara waliouza mafuta kwa bei iliyozidi bei kikomo.

iv. Kusambazwa kwa mafuta yanayokidhi viwango vya ubora kwani asilimia kubwa ya sampuli za mafuta zilizochukuliwa na kupimwa, zilikidhi viwango vya ubora.

v. Ongezeko la matumizi ya LPG linalochangiwa na uhamasishaji wa matumizi ya nishati hiyo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia.

vi. Upatikanaji wa uhakika wa mafuta kwa kufuatilia kwa karibu mahitaji ya soko na mipango ya uagizaji wa mafuta.

vii. Kuongezeka kwa idadi ya vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini kutokana na uhamasishaji wa ujenzi wa vituo vya mafuta vyenye gharama nafuu katika maeneo ya vijijini bila kuathiri viwango vya afya, usalama na mazingira. Ongezeko hili la vituo vya vijijini limeboresha upatikanaji wa mafuta katika maeneo hayo.

viii. Ulinzi wa wafanyabiashara wa mafuta na Mapato ya Serikali kupitia mpango wa kuweka vinasaba kwenye mafuta ili kuzuia usambazaji wa mafuta haramu au yasiyozingatia sheria na kanuni zinazosimamia bishara ya mafuta nchini.

# 13. CHANGAMOTO KATIKA SEKTA NDOGO YA MAFUTA

Sekta ndogo ya mafuta inaendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo:

i. Kutokuwepo kwa Ghala Kuu la kupokelea mafuta husababisha muda mrefu wa upokeaji wa mafuta kutoka kwenye meli za mafuta, gharama za juu kutokana na meli kushindwa kupakua mafuta kwa wakati, na uwezo mdogo wa bandari kupokea meli zaidi ndani ya muda uliowekwa.

ii. Uhitaji wa kuongezwa kwa uwekezaji katika vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini ili kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa mafuta ya petroli na kwa gharama elekezi, sambamba na kuzingatia viwango vya afya, usalama na mazingira.

iii. Uwepo wa mafuta yasiyolipiwa kodi katika soko la Tanzania Bara (hususan yale ambayo yalitakiwa kupelekwa nchi za jirani) bado ni changamoto kwani inaharibu ushindani katika soko na kusababisha upotevu wa mapato stahiki kwa Serikali.

iv. Kutoweza kupokea meli kubwa katika gati za Kurasini na hivyo kushindwa kupata faida za kiuchumi kwa kuagiza mzigo mkubwa wa mafuta kwa mara moja.

v. Gharama kubwa za kuanza kutumia gesi ya kupikia huzuia utumiaji wa gesi hiyo miongoni mwa watu wa kipato cha chini.

vi. Ujazaji wa mitungi ya gesi ya kupikia katika maeneo ambayo hayajaruhusiwa kisheria.

# 14. MTAZAMO WA BAADAYE WA SEKTA NDOGO YA MAFUTA

Matumizi ya mafuta yanaendelea kuongezeka nchini Tanzania na nchi jirani hivyo kuna umuhimu wa kuongeza na kuboresha miundombinu ya kupokea na kuhifadhi mafuta ili kuweza kupokea meli kubwa zaidi na kupakua mafuta kwa haraka. Ili kufanikisha hili, Serikali inatarajia kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha bidhaa za mafuta. Mkakati huu unalenga kukidhi ongezeko la mahitaji ya mafuta ndani ya nchi na kuhudumia nchi jirani zinazotegemea bandari za Tanzania katika kuagiza mafuta.

Waendeshaji wa vituo vya mafuta na maghala ya kupokea na kuhifadhi mafuta wanafanya taratibu za kufunga mifumo maalum ya kutambua kiwango cha mafuta kwenye maghala (*Automatic Tank Gauging Systems - ATGs*). Mifumo hii ya kidijitali itaiwezesha Mamlaka kufuatilia na kusimamia ipasavyo upatikanaji wa bidhaa za mafuta nchini.

Katika kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi na matumizi bora ya maliasili zetu ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni, Serikali imekuwa ikihimiza matumizi ya gesi asilia kwenye magari. Idadi ya magari yanayobadilishwa na kuanza kutumia gesi hiyo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Aidha, kuna ongezeko la uagizaji wa magari ya umeme na magari yanayotumia mafuta na umeme, hali inayoweza kupunguza matumizi ya mafuta. Hata hivyo, kutokana na teknolojia hizi kuwa mpya na magari hayo kuwa ya gharama kubwa ikilinganishwa na magari ya dizeli na petroli, matumizi ya mafuta ya petroli na dizeli yanatarajiwa kuendelea kuongezeka katika kipindi cha muda wa kati.

# 15. HITIMISHO

Kwa ujumla, sekta ndogo ya mafuta katika mkondo wa kati na chini imefanya vizuri kutokana na uboreshaji na ongezeko la uwekezaji katika miundombinu, usimamizi madhubuti wa manunuzi ya mafuta kupitia Mfumo wa BPS na kazi za kiudhibiti zinazofanywa na EWURA. Ili kuwa na mafanikio endelevu, Mamlaka itaendelea kusimamia utendaji wa sekta hii, kuhakikisha upatikanaji endelevu wa bidhaa za mafuta katika ubora unaotakiwa na hivyo kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi. Katika siku za usoni, Mamlaka inatarajia:

i. Kuhamasisha uwekezaji kwa kuandaa na kupitia nyenzo za udhibiti na kuishauri Serikali kuhusu sera na mikakati inayohitajika ili kuvutia uwekezaji katika uendelezaji na uboreshaji wa miundombinu ili kuongeza uwezo wa kuhifadhi, kurahisisha upakuaji mafuta na kuweza kupokea meli kubwa zaidi zitakazoongeza ufanisi katika uagizaji wa mafuta nchini.

ii. Kuimarisha usimamizi wa upokeaji na usambazaji wa mafuta kwa kutumia mifumo ya za kisasa ya kupata taarifa sahihi na kwa wakati halisi kuhusu mafuta yaliyopokelewa kwenye maghala, yaliyosambazwa au kusafirishwa kwenda nje ya nchi na yaliyopo katika vituo vya mafuta.

iii. Kuimarisha utekelezaji wa sheria kwa kuongeza ufuatiliaji wa utii na utekelezaji wa sheria, kanuni na taratibu ili kuhakikisha wafanyabiashara wanafuata sheria, taratibu za usalama na udhibiti wa ubora.

iv. Kupitia au kutengeneza nyenzo za udhibiti zitakazohamasisha uwekezaji katika vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini na maeneo mengine ambayo hayajafikiwa na huduma za mafuta ili kuboresha upatikanaji wa mafuta.

v. Kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali katika kupambana na shughuli haramu kama vile uingizaji wa bidhaa za mafuta kwa magendo, kujaza mitungi ya gesi ya kupikia kinyume cha sheria, na vitendo vingine vinavyodhoofisha ushindani wa haki na kuhatarisha mazingira na usalama wa watumiaji wa bidhaa za mafuta na umma kwa ujumla.

vi. Kuhamasisha matumizi ya gesi ya kupikia ikiwa ni njia mojawapo ya kutunza mazingira na afya.

vii. Kuboresha mfumo wa uagizaji wa mafuta ili kuongeza ufanisi, kupunguza gharama, na kuwezesha mafuta kupatikana kwa uhakika.

Kwa kuzingatia maeneo hayo, Mamlaka inalenga kudumisha mafanikio ya sasa na kuboresha zaidi sekta ndogo ya mafuta.